

## **MAELEZO YA MRADI**

### **MRADI WA USIMAMIZI ENDELEVU WA MATUMIZI YA ARDHI YA BONDE LA ZIWA NYASA (SUSTAINABLE LAND MANAGEMENT OF LAKE NYASA CATCHMENT IN TANZANIA PROJECT)**

#### **1. Utangulizi**

Bonde la Ziwa Nyasa ni Ziwa muhimu kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa watu takribani zaidi ya Milioni moja wanaoishi kwenye bonde la ziwa hili. Ziwa hilo lina aina mbalimbali za bioanuai wakiwemo aina 800 za samaki ambao hawapatikani sehemu nyingine duniani. Hata hivyo, bioanuai hizo zinatishiwa kutokana na matumizi yasiyo endelevu.

Shughuli kubwa zinazofanywa na wakazi wa bonde la Ziwa Nyasa ni: kilimo, uchimbaji wa madini, uvuvi na usafirishaji wa mazao ya kilimo pamoja na maliasili zinazovunwa katika bonde hilo ziwani.

#### **2. Jina la mradi:**

Usimamizi wa Matumizi Endelevu ya Ardhi ya Bonde la Ziwa Nyasa (**GEF ID 5691 – UNEP SUSTAINABLE LAND MANAGEMENT OF LAKE NYASA CATCHMENT IN TANZANIA**)

#### **3. Lengo la mradi**

Mradi una malengo yafuatayo:-

- i. Kukabiliana na uharibifu wa mazingira katika bonde la Ziwa Nyasa ambao umetokana na shughuli za kibinadamu zisizo endelevu. Shughuli hizo ni pamoja na; kulima kandokando ya kingo za mito na vyanzo vya maji, kulima katika miteremko ya milima, kujihusisha na Uvuvi haramu unaohusisha matumizi ya zana zisizoruhusiwa kisheria, kuchoma moto ovyo, kukata miti ovyo kwa ajili ya mkaa na kuni pamoja na kuchimba madini kwa njia isiyo endelevu.
- ii. Kuboresha maisha ya jamii inayozunguka bonde hilo kwa kufanya shughuli mbadala zinazozingatia hifadhi ya ardhi na mazingira zinazoboresha kipato, na hivyo kupunguza utegemezi mkubwa wa maliasili zilizopo katika bonde hilo.

#### **4. Shughuli za Mradi:**

Mradi unamaeneo “**Components**” (3) matatu ya utekelezaji ambayo ni:-

- i) Kuimarisha uwezo wa usimamizi endelevu wa ardhi katika eneo la Mradi. (*Strengthening capacities at catchment level for SLM*);
- ii) Kujumuisha mifumo ya usimamizi endelevu wa Ardhi katika Bonde (*Integrated Catchment management through SLM systems*); na

- iii) Kuwezesha na kuhusianisha Sera na Mikakati ya Kitaasisi katika usimamizi wa Matumizi endelevu ya Ardhi katika Bonde la Ziwa Nyasa (*Enabling Policy and Institutional Framework*).

Shughuli zinazofanyika katika Mradi wa Hifadhi ya Mazingira kulingana na maeneo matatu “components” ya utekelezaji ni:-

**Component 1:** Kujenga uwezo katika hifadhi ya mazingira katika bonde la Ziwa Nyasa (*Strengthening capacities at catchment level for SLM*)

**Shughuli:**

- 1.1** Kubaini na kufanya tathmini ya shughuli za matumizi ya ardhi katika wilaya zilizokusudiwa (*Conduct baseline mapping and assessment of land use activities in targeted districts*);
- 1.2** Kuwa na mpango bora wa matumizi ya ardhi katika bonde la Ziwa Nyasa (*Catchment/Village land use plans developed*);
- 1.3** kuelimisha na kukuza uelewa kuhusu mbinu bora na endelevu za usimamizi wa ardhi (*Awareness programme on sustainable land management practices developed and communities mobilized*);
- 1.4** Kujenga uwezo na kuimarisha Halmashauri zote za Wilaya zilizopo katika bonde la Ziwa Nyasa kuhusu usimamizi endelevu wa Bonde la Ziwa Nyasa (*Capacity building and strengthening of district council on planning and catchment management*);

**Component 2:** Kuwa na mifumo jumuishi ya usimamizi bonde la Ziwa nyasa kwa kutumia mbinu endelevu za usimamizi ardhi (*Integrated Catchment management through SLM systems*)

**Shughuli:**

- 2.1** Kuhakikisha kilimo endelevu zinazingatiwa kwa kuhifadhi na kutenga maeneo yanayolimwa (*Land rehabilitation/ conservation/ protection measures implemented on cultivated land*);
- 2.2** Maeneo ya Ziwa yaliyoharibiwa na vyanzo vya maji yanakarabatiwa na kuhifadhiwa (*Degraded lake catchment areas and water sources rehabilitated/conserved*);
- 2.3** Mbinu za kilimo bora cha hifadhi kutekelezwa katika ardhi inayofaa kwa kilimo (*Techniques on conservation agriculture implemented on arable land*);
- 2.4** Njia mbadala ya kuongeza kipato kubainishwa na kutekelezwa (*Alternative income generating activities identified and implemented*);

- 2.5** Maeneo yaliyotelekezwa kutokana na shughuli za uchimbaji kukarabatiwa kwa kupandwa miti (*Degraded Mined land rehabilitated through reforestation*); na
- 2.6** Mbinu za asili za kuhifadhi ardhi na mazao ya chakula kuendelezwa (*Adoption of SLM practices and conservation of indigenous food crop varieties increased*).

**Component 3:** Uwezeshaji kwa mfumo wa Kisera na kitaasisi (*Enabling Policy and Institutional Framework*)

**Shughuli:**

- 3.1** Kuhimarisha Utekelezaji wa sheria ndogo ndogo katika serikali za mitaa kwa ajili ya usimamizi wa bonde (*Enforcement on by-laws for catchment management by local authorities*); na
- 3.2** Kuanzisha kamati za kisekta/kiwizara kusimamia bonde (*Inter-ministerial committee on Lake Nyasa established*).

**5. Maeneo Mradi unapotekelezwa:**

Mradi unasimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais na utatekelezwa na Halmashauri za Wilaya tano (5) zilizoko kwenye Bonde la Ziwa Nyasa, pamoja na taasisi za Serikali na zisizo za Kiserikali. Halmashauri za Wilaya zinazoshiriki kutekeleza mradi huu ni pamoja na Ludewa, Kyela, Makete, Nyasa na Mbinga. Aidha, wadau wengine watakaoshiriki katika kutekeleza mradi huu ni pamoja na Chuo kikuu cha kilimo cha Sokoine (SUA); Tume ya Usimamizi wa Matumizi Bora ya Ardhi, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Maji kuitia Bodi ya Maji ya Bonde la Ziwa Nyasa, Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na NGOs zinazojishughulisha na masuala ya hifadhi ya Mazingira zilizoko katika Bonde la Ziwa Nyasa.